TUME YA KIKRISTO YA HUDUMA ZA JAMII
KAMATI YA MITIHANI YA PAMOJA KANDA YA KASKAZINI

MTIHANI WA UTAMIRIFU KIDATO CHA SITA, 2026

121/1 **KISWAHILI 1**

Muda: Saa 3 **Jumatano, 25 Februari 2026 Asubuhi**

Maelekezo

1. Mtihani huu una **sehemu A** na **B,** zenye jumla ya **maswali nane (8)**
2. Jibu maswali yote katika sehemu **A** na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu **B**. swali la **tano (5)** ni la lazima.
3. Zingatia **maelekezo** ya **kila sehemu** na ya kila swali
4. Simu za **mkononi** na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 40)

Fanya maswali **yote** katika sehemu hii

1. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata:

Namuona yu shambani
Analima
Mavuno si yake
Ni ya mume wake

Namuona kiwandani
Pia maofisini
Ya kazini
Hamkani
Anabaguliwa
Na anaonewa

Namuona yu nyumbani
Mpishi wa jikoni
Yaya yeye
Dobi yeye
Hakuna malipo
Likizo haipo

Namuona kitandani
Yu uchi maungoni
Ni mrembo
Kama chombo
Chenye ushawishi
Mzima utashi

Namuona mkekani
Yumo uzanini
Anapumua
Augua
Kilio cha kite
Cha mpiga pute

Kwanini mwanamke
Ni yeye peke yake
Anyimwaye
Heshimaye
Haki anakosa
Kwa kweli ni kosa

Maswali

(a) Kwa maneno yasiyozidi **matatu**, andika kichwa cha shairi hili.
(b) Eleza maana ya maneno yafuatayo:
(i) Kilio cha kite (ii) Yaya (iii) Chombo cha starehe (iv) Dobi
(c) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu mbili kufafanua jibu lako.
(d) Kwanini mwandishi anamuona mwanamke hana likizo?
(e) Unafikiri mshairi anatoa ujumbe gani kwa hadhira yake?

2. Makosa ya kisarufi na kimantiki hayaepukiki katika jamii ya waswahili. Thibitisha dai hili kwa mifano. Hoja **tano (5).**
3. Dhima mojawapo ya vitenzi vya Kiswahili ni kuonesha hali mbalimbali. Kwa kutumia mifano, fafanua hali mbalimbali za vitenzi vya Kiswahili. Hoja **tano (5).**
4. Mtumiaji yoyote wa lugha huongozwa na utaratibu husika. Kwa kutoa mifano onesha ni mambo yapi mtumiaji wa lugha huyazingatia wakati wa kutumia lugha. Hoja **tano (5).**

SEHEMU B (alama 60)

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii. Swali la **5 ni la lazima.**

5. "Taaluma ya tafsiri ina uhusiano na taaluma nyingine". Kwa kutoa mifano kuntu zifafanue taaluma nyingine zinazohusiana na tafsiri. Hoja **sita (6)**.
6. Andika barua kwa mhariri wa gazeti la uhuru ukiwaeleza wanafunzi namna ya kufanya ili kupata ufaulu mzuri kwenye mitihani yao. Jina lako ni Nyanya Chungu wa Sanduku la Posta 222 Buzuruga.
7. "Toka enzi za uhuru hadi sasa lugha ya Kiswahili imepata mafanikio makubwa ndani na nje ya Tanzania". Thibitisha dai hili kwa kutoa hoja **sita (6)**.
8. Kushamiri kwa Kiswahili sanifu kunasababisha lahaja nyingine kudumaa na nyingine kutoweka kabisa. Thibitihsa kauli hii kwa hoja **sita (6)**.